**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Nne – Tarehe 21 Februari, 2022**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Mwaka 2021/2022.**

Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Mwaka 2021/2022.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

1. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

   Wakati Serikali ikijikita katika kuwekeza zaidi kwenye Uchumi wa Buluu, wananchi wanaamini kwamba, Serikali itaendelea kukipa kipaumbele kilimo cha juu na uvuvi. Pamoja na adhma hiyo, kumekuwa na kero ya muda mrefu ya kuvamiwa na chumvi kwenye bonde la kilimo cha juu katika ukanda wa bahari wanaoutumia wananchi wa Mjananza na shehia nyengine za jimbo la Pandani.

   (a) Je, Serikali imechukua hatua gani kuzuia uvamizi wa chumvi katika bonde la kilimo cha juu katika ukanda wa bahari ya mashariki ya Pemba.

(b) Je, ni lini Serikali itajenga tuta au suluhisho jengine kuzuia uvamizi wa chumvi kwenye bonde la kilimo cha juu la watu wa Mjanaza Pemba.

**<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>**

26. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Sheria na Kanuni za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imepiga marufuku kwa wenye punda na ng'ombe pamoja na mbuzi kuchunga au kuendesha magari ya ng'ombe katika maeneo ya miji, hata hivyo marufuku hiyo imekuwa ikipuuzwa na wenye mifugo hiyo hali ambayo inaleta usumbufu mkubwa kwa wananchi wengine.

(a) Je, Serikali inamkakati gani wa kudumu kukabiliana na tatizo hili sugu.

(b) Ni wanyama wangapi wamekamatwa katika Manispaa tatu za Mkoa wa Mjini Magharibi kwa kipindi cha Januari – Juni, 2021 kutokana na kukiuka Sheria na Kanuni.

32. MHESHIMIWA NASSOR SALUM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali ya Mkoa wa Mjini Magharibi iliwahi kutoa agizo kuwa shughuli za muziki na ngoma ziwe zinamalizika saa 6:00 usiku. Hata hivyo, inaonekana agizo hilo hivi sasa halifuatwi,kwa kuwa kelele za miziki zinasikika zaidi ya muda huo na kuleta kero kwa wananchi.

(a) Je, agizo la kupiga marufuku shughuli za ngoma na muziki zaidi ya saa 6:00 usiku limefutwa.

(b) Kama halijafutwa, Serikali ya Mkoa wa Mjini Magharibi ipo tayari kutoa agizo jengine la ukumbusho na kusimamia utekelezaji wake kwa watakaokaidi.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

4. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

   Kwa kuwa Tanzania Bara ipo Mamlaka moja ya kukusanya mapato (TRA), na kwa kuwa Zanzibar zipo Mamlaka mbili za kukusanya mapato (ZRB na TRA), na kwa kuwa yapo malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara wa Zanzibar juu ya kukatwa kodi mara mbili wanaposafirisha bidhaa zao kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara.

   Je, ni ipi kauli ya Serikali kwa wafanyabiashara wa Zanzibar juu ya kadhia hii.

**Ofisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji:**

119. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji.

   Jimbo la Kiembesamaki ni miongoni mwa majimbo yenye taasisi nyingi za kiuchumi zinazomilikiwa na wawekezaji wa nje na ndani ya nchi. Kwa bahati mbaya wawekezaji hao hawafuati baadhi ya sheria hasa Sheria za Utumishi wa Umma na kupelekea wananchi wa sehemu husika kukosa faida za moja kwa moja kwa wawekezaji hao ikiwemo ajira.

   (a) Je, Serikali inatambua changamoto hiyo.

   (b) Ni hatua zipi Serikali kupitia taasisi husika wamezichukua kuondosha changamoto hiyo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

58. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

   Serikali inaendelea kuboresha huduma ya maji mijini na vijijini kwa kasi inayostahili pongezi. Hata hivyo, katika usomaji wa mita na ukadiriaji wa bili, kumekuwa na malalamiko makubwa hasa katika jimbo la Pandani kwa sababu bili za maji zinazotolewa, mara nyingi huwa sio sahihi na za uonevu. Mita nyingi hazisomi sahihi.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasilisha malalamiko ya watu wanaoonewa au kuwekewa bili zisizo sahihi na ni utaratibu upi wa kuwafidia.

(b) Je, ni lini Serikali itatumia risiti zinazodumu kwa muda mrefu zaidi ukilinganisha na za sasa ambazo zinafutika ndani ya siku chache.

(c) Je, Serikali inawahakikishiaje wananchi kwamba utaratibu wa sasa wa kukadiria bili hauna chembe ya rushwa na ni lini Serikali itaanza kutumia mfano wa TUKUZA kwa umeme katika kulipia huduma ya maji.

62. MHESHIMIWA MTUMWA PEYA YUSSUF (Jimbo la Bumbwini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Wakati wa ujenzi wa barabara ya Bububu - Mahonda - Mkokotoni eneo la Mkadini miundombinu ya maji iliharibiwa na haijarudishwa.

(a) Je, ni nani mwenye dhamana ya kuirudisha miundombinu hiyo.

(b) Kwa nini mpaka sasa haijarudishwa.

63. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Naipongeza Serikali kwa kutoa kauli kuhusiana na azma ya kuwapelekea nguzo za umeme bure wananchi wa Zanzibar na kuifanya huduma isiwe kikwazo. Lakini licha ya hatua hiyo, bado kumekuwa na malalamiko kwa wananchi wa kisiwa cha Pemba hasa vijijini kuhusu kuchukua muda mrefu wa uungwaji wa umeme baada ya wananchi kukamilisha utaratibu wa malipo.

(a) Je, ni sababu gani Shirika la Umeme linashindwa kutoa huduma za uungaji wa umeme kwa wakati mpaka linalalamikiwa na wateja.

(b) Ni lini Shirika la Umeme litaondoa kadhia hiyo hasa kwa wananchi wa vijijini ambako kumekuwa na mwamko mkubwa wa wananchi kufuata huduma hiyo kwa wakati.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

66. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Pamoja na jitihada za Serikali za kuboresha afya ya mama na mtoto, bado kumekuwa na shida kubwa ya usafiri katika shehia zote za jimbo la Pandani kwa wanawake wajawazito na wagonjwa wasiojiweza kwa sababu vituo vya afya viko mbali na, hasa wakati wa usiku, husababisha vifo na athari nyengine zisizo za lazima.

(a) Je, Serikali ina mipango ipi ya dharura na ya kudumu ya kuviwezesha kiusafiri vituo vya afya kwa kila shehia.

(b) Je, ni lini Serikali itaanzisha mpango wa kliniki zinazotembea (mobile clinics) katika vijiji vya jimbo la Pandani.

74. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto.

Jengo la Kituo cha Afya cha Kojani ni muhimu sana kwa wakazi pamoja na watembezi wa kisiwa hicho. Kwa kuwa tangu kuanza kufanyakazi kwa kituo hicho hadi leo hii kumekuwa na ukosefu wa uzio wa tofali pamoja na uchakavu wa mambo muhimu kama vile mafeni 6, kipoza hewa (AC) ya dawa na taa.

Je, ni lini Serikali itajenga uzio pamoja na kuwapatia vifaa hivyo muhimu vilivyochakaa.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

9. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Zanzibar imepitia katika historia kubwa ya maendeleo ya mpira wa miguu kitaifa, kikanda na hata kimataifa.

Je, Wizara itakubaliana na mimi kwamba kama zilivyo nchi nyengine duniani ipo haja ya kuanzisha makumbusho ya historia ya mpira wa miguu Zanzibar, ambapo pamoja na umuhimu huo

makumbusho haya yatakuwa miongoni mwa vyanzo vya kuiongezea Serikali mapato.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

35. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na ongezeko la wafanyabiashara kusafirisha mazao mbali mbali kwa kupeleka nje ya nchi. Bidhaa hizi zikiwa ni za kutoka au za kuingia huekewa utaratibu wa kuchelewa au kuwahishwa katika eneo la bandari zetu na baadhi ya bidhaa hizo huhitaji kuwekwa katika mazingira ya ubaridi ili zisipoteze thamani yake.

(a) Katika bandari za Zanzibar mpaka sasa tunayo maeneo mangapi yenye miundombinu ya sehemu maalum zenye ubaridi (cool room).

(b) Kama zipo, Je, zina uwezo wa kuhifadhi tani ngapi kwa wakati mmoja.

(c) Na kama hatuna, Je. inapotokea uharibifu wa mazao, ni Serikali au nani anaepaswa kulipia uharibifu katika eneo la bandarini.

42. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Juhudi za kujenga barabara mbali mbali za Zanzibar zinakwenda sambamba na kuwalipa fidia ya thamani halisi ya mali za wananchi wetu pamoja na kuwalipa kwa wakati. Hata hivyo, kuna madai mengi ya kutolipwa kwa fidia kwa wananchi waliochukuliwa maeneo yao, ikiwa ni pamoja na njia ya Pagali.

Je, ni lini wananchi hao wa njia ya Pagali watalipwa fidia zao.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

87. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tumekuwa tukishuhudia jitihada mbali mbali zinazochukuliwa na Serikali zetu mbili za Tanzania, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya kuboresha elimu ya juu, lakini hadi hivi sasa kuna wasimamizi wa mitihani ya kidato cha nne wa mwaka 2020 hawajalipwa malipo yao.

(a) Je, ni lini watalipwa malipo hayo hasa ukizingatia kazi kama hiyo itafanyika tena hivi karibuni.

(b) Je, hatuoni kuwa tunawavunja moyo.

(c) Je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayo habari hii kuwa wasimamizi wa mitihani bado hawajalipwa.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

109. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Suala la uharibifu wa mazingira ikiwemo ukataji holela wa mikoko na mazalia ya samaki (matumbawe) linaathiri sekta ya maendeleo ya uvuvi wa samaki.

(a) Je, ni hatua gani zimechukuliwa kwa wale waliokamatwa na uharibifu huo.

(b) Je, Wizara inakumbana na changamoto zipi na ina mpango gani wa ziada wa kuliondoa tatizo hili.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

127. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Katika malengo yake ya Bajeti ya mwaka 2021/2022, Shirika la Nyumba linakusudia kupandisha kodi za nyumba zake kuanzia

mwezi Septemba, 2020/2021, kwa kiwango cha asilimia sitini ya bei halisi ya soko kulingana na eneo nyumba ilipo.

(a) Je, Mhe. Waziri lengo hili mpaka sasa lipo katika hatua gani.

(b) Je, ni kiasi gani ambacho Shirika la Nyumba linakodisha nyumba zao kwa sasa.

**<u>Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:</u>**

101. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Mikate ya boflo ina “brand” ya Zanzibar na imekuwa maarufu duniani.

(a) Je, kuna hatua zozote zinazochukuliwa kufanya ukaguzi wa bekari za mikate kuona mazingira ya usafi na ubora (kiwango) yanazingatiwa.

(b) Ni kiasi gani cha usalama wa watumiaji unazingatiwa na wauzaji wa mikate ya boflo mtaani.

(c) Je, kwa sasa Serikali haioni kuna haja mikate ya boflo nayo kuhifadhiwa kwenye mifuko ya plastiki.

## III. <u>HOJA ZA KAMATI:</u>

**<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi ya Mwaka 2021/2022:</u>**

Ripoti ya Kamati ya Uchumi ya Mwaka 2021/2022.

**<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Mwaka 2021/2022.</u>**

Ripoti ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**21 Februari, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**<u>KATIBU WA BARAZA</u>.**